**TUMAINI (2002) LADIES VENTURE (TLV)**

***Our Motto: "Unity and Empowerment"***

# KATIBA YA TUMAINI (2002) LADIES VENTURE

(TLV'S CONSTITUTION)

**2nd Edition revised in Kiswahili 2023**

# Contents


KATIBA YA TUMAINI (2002) LADIES VENTURE ........ 1

1.0 JINA ........ 3

2.0 ANWANI ........ 3

3.0 OFISI ........ 3

4.0 TAFSIRI ........ 3

5.0 MALENGO ........ 4

6.0 UANACHAMA ........ 5

7.0 IDADI YA WANACHAMA ........ 5

8.0 SIFA ZA WANACHAMA ........ 5

9.0 WAJIBU WA MWANACHAMA ........ 6

10.0 UKOMO WA UANACHAMA ........ 7

11.0 ATHARI YA UKOMO WA UANACHAMA ........ 8

12.0 HAKI YA MWANACHAMA ........ 10

13.0 MWANACHAMA MPYA ........ 11

14.0 UONGOZI WA CHAMA ........ 12

15.0 MUDA WA UONGOZI ........ 12

16.0 WAJIBU WA VIONGOZI ........ 12

17.0 UKOMO WA UONGOZI ........ 14

18.0 KAMATI TENDAJI ........ 15

19.0 MIKUTANO ........ 16

20.0 FEDHA ZA CHAMA ........ 17

21.0 AINA ZA MICHANGO ........ 17

22.0 MIKOPO ........ 19

23.0 MIRADI YA CHAMA ........ 20

24.0 MALI ZA CHAMA ........ 20

25.0 KUVUNJWA KWA CHAMA ........ 20

26.0 MABADILIKO YA KATIBA ........ 21

27.0 LUGHA YA KATIBA ........ 21

## 1.0 JINA

1.1 Jina la chama litakuwa **TUMAINI (2002) LADIES VENTURE** na kifupi chake kitajulikana kama **TLV.**

## 2.0 ANWANI

2.1 Anwani ya Chama itakuwa: S. L. P. 5198, Dar Es Salaam, Tanzania; na anwani ya barua pepe ya Chama itakuwa info@tlv.co.tz

## 3.0 OFISI

3.1 Ofisi ya Chama zitakuwa Dar es Salaam, Tanzania.

## 4.0 TAFSIRI

4.1 Isipokuwa pale Katiba hii itakapotoa maelezo mbadala, vinginevyo tafsiri za baadhi ya maneno katika Katiba hii itakuwa ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| **"Chama"** | ina maana **TUMAINI (2002) LADIES VENTURE (TLV).** |
| **"Hisa"** | ina maana Hisa za Chama. |
| **"Katiba"** | ina maana ya Katiba ya Chama kama ilivyopitishwa na wanachama waanzilishi katika kikao chao cha kwanza na kama itavyorekebishwa na mkutano halali. |
| **"Kamati Tendaji"** | ina maana ya uongozi wa Chama ambao ni Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina. |

**"Mkutano"** ina maana Mkutano wa Chama kama ilivyoainishwa kwenye Katiba.

**"Mrithi"** ina maana ya aliyetajwa kama mrithi kwenye kumbukumbu za Mwanachama husika.

**"Mwanachama"** ina maana ya Mwanachama hai wa **TUMAINI (2002) LADIES VENTURE** ambaye amelipa kiingilio na michango yake kwa wakati na anahudhuria mikutano ya Chama iliyopo kwa mujibu wa Katiba.

**"Mwaka wa Fedha"** ina maana ni kipindi cha kuanzia mwezi Januari na kuishia mwezi Disemba ya mwaka huo huo.

## 5.0 MALENGO

Malengo ya Chama hiki ni kama ifuatavyo:

5.1 Kuwaweka wanachama pamoja kwa nia ya kufahamiana, kujenga urafiki na udugu.

5.2 Kuwawezesha wanachama kuendesha mpango wa kuweka na kukopa wakilenga katika kuboresha maisha yao kiuchumi na kijamii.

5.3 Kuwaunganisha wanachama na taasisi nyingine ambazo kutokana na malengo ya Chama zitakiwezesha Chama kufikia malengo yake.

5.4 Kuwekeza katika shughuli za kiuchumi ili kuinua mfuko wa Chama.

5.5 Kuwawezesha wanachama kusaidiana katika nyakati za shida na raha.

## 6.0 UANACHAMA

6.1 Kutakuwa na uananchama wa aina tatu (3) ambao ni:

a) wanachama waanzilishi: ni wanachama nane waanzilishi wa TLV (na ndiyo waliopitisha Katiba hii);

b) wanachama wa kawaida: ni wanachama ambao watajiunga na TLV kwa kukubaliana na wanachama waanzilishi; na

c) wanachama wa heshima: ni wanachama ambao kwa mujibu wa wadhfa wao katika jamii, wanachama waanzilishi wanaweza kukubalia kuwapa uanachama wa TLV.

## 7.0 IDADI YA WANACHAMA

7.1 Chama kitakuwa na wanachama wasiozi ishirini (20).

## 8.0 SIFA ZA WANACHAMA

8.1 Mwenye umri zaidi ya miaka kumi na nane (18).

8.2 Mwenye akili timamu.

8.3 Anayeheshimu kanuni na masharti mbalimbali kama yalivyoainishwa katika Katiba na nyaraka nyingine za Chama.

8.4 Anayetimiza wajibu wa mwanachama kama ilivyoainishwa na Katiba hii.

8.5 Mwenye nidhamu na mahusiano mazuri na wanachama wenzake.

## 9.0 WAJIBU WA MWANACHAMA

Mwanachama atakuwa na wajibu ufuatao:

9.1 Kulipa kiingilio (entry fee) cha kujiunga na uananchama cha Shilingi laki tano (Tshs.500,000/-) au itakavyo badilika kama itakavyoamuliwa na wanachama au kwenye Kanuni za Fedha za Chama.

9.2 Kununua walau hisa zenye thamani ya Shilingi laki moja (100,000/-) kila mwezi kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Chama.

9.3 Kulipia mchango wa Jamii kama itakavyo amuliwa na wanachama au kwenye Kanuni za Jamii za Chama.

9.4 Kuchangia michango kwa wakati.

9.5 Kukopa na kurejesha mikopo kwa mujibu wa Katiba, Kanuni na taratibbu zilizowekwa.

9.6 Kuhudhuria mikutano na kushiriki shughuli za Chama.

9.7 Mwanachama anawajibika kuhudhuria vikao visivyo pungua sita kwa mwaka. Mwanachama

atakayeathiriwa na ibara hii atajadiliwa na Kikao cha mwisho wa mwaka. Kwa mwanachama aliyeko nje ya nchi (Tanzania) au nje ya mkoa wa Dar es Salaam atatakiwa kuhudhuria walau kikao kimoja cha ana kwa ana.

9.8 Kutunza siri za chama.

9.9 Kuzifahamu na kuzifuata Sheria, Katiba, Kanuni na taratibu za Chama.

9.10 Kulinda na kutunza Katiba, kanuni, heshima na amani ya Chama.

## 10.0 UKOMO WA UANACHAMA

Mwanachama atakoma kuwa Mwanachama iwapo:

10.1 Atapoteza sifa za uanachama.

10.2 Ataacha mwenyewe.

10.3 Atafariki.

10.4 Atatangazwa mufilisi.

10.5 Atahukumiwa na chombo chenye mamlaka ya kisheria kwa kosa la jinai linalihusiana na fedha au uaminifu.

10.6 Atafukuzwa uanachama, kama itakavyo amuliwa na wanachama waanzilishi.

10.7 Hajahuduria mikutano mitatu (3) mfululizo bila sababu za msingi na bila taarifa kwa Uongozi wa Chama au/na mwenyeji wa kikao husika.

10.8 Atashindwa kununua hisa angalau ya Shilingi laki moja (Tshs.100,000/-) kwa miezi mitatu mfululizo.

## 11.0 ATHARI YA UKOMO WA UANACHAMA

11.1 Endapo mwanachama atakoma uanachama:

a) Atarudishiwa thamani ya hisa zake zote na faida yote inayotokana na hisa zake baada ya kurejeshwa kwa madeni mwisho wa mwaka wa kalenda; au

b) Akiridhia hisa zake zitawekwa wazi kwa mauzo kwa wanachama wote kama hisa za ziada.

Ilimradi mwanachama ambaye hisa zake zinawekwa wazi kwa mauzo kwa mujibu wa ibara ndogo ya 11.1(b) hapo juu hatastahili faida katika hisa zake.

11.2 Endapo mwanachama atakiuka masharti ya uanachama na kuangukia kwenye ukomo wa mwanachama baada ya kupewa onyo basi atarejeshewa thamani ya hisa zake zote na faida yote inayotokana na hisa zake mwisho wa mwaka wa kalenda baada ya kurejeshwa kwa madeni yote. Ilimradi kama uanachama wake utakoma kutokana na kukiuka kwa masharti ya uanachama, Chama kitakuwa na mamlaka ya kuanua kumrejeshea stahili zake hata kabla ya mwisho wa mwaka

11.3 Endapo mwanachama amefukuzwa kwenye chama:

a) Atarejeshewa thamani ya hisa zake pamoja na asilimia sabini ya faida inayotokana na hisa zake mwisho wa mwaka wa kalenda.

b) Akiridhia hisa zake zitawekwa wazi kwa mauzo kwa wanachama wote kama hisa za ziada.

Ilimradi mwanachama ambaye hisa zake zinawekwa wazi kwa mauzo kwa mujibu wa ibara ndogo ya 11.3(b) hapo juu hatastahili faida katika hisa zake.

11.4 Endapo mwanachama atafariki mrithi wake atapewa thamani ya hisa zake (yaani hisa za Mwanachama aliyefariki), zote na faida yote inayotokana na hisa zake mwisho wa mwaka wa kalenda baada ya kurejeshwa kwa madeni yote, endapo yapo. Thamani ya hisa zake zote na faida yote inayotokana na hisa zake mwisho wa mwaka wa kalenda baada ya kurejeshwa kwa madeni yote, Chama kitakuwa na mamlaka ya kuamua kumrejeshea stahili zake hata kabla ya mwisho wa mwaka.

11.5 Endapo mwanachama atakoma uanachama kwa sababu ya afya ya akili, kuhukumiwa kwa mujibu wa ibara ya 10.5 au kufilisiwa atarejeshewa thamani ya hisa zake zote na faida yote inayotokana na hisa zake mwisho wa mwaka wa kalenda baada ya kurejeshwa kwa madeni yote. Ilimradi kama uanachama wake utakoma kutokana na kurukwa na afya ya akili, Chama kitakuwa na mamlaka ya kuamua kurejesha stahili zake kwa mrithi wake hata kabla ya mwisho wa mwaka.

11.6 Mwanachama akikoma uanachama kwa sababu zozote zile zilizoanishwa kwenye Katiba hii hatorejeshewa pesa za Mfuko wa Jamii, Faini wala Fedha ya kiingilio.

11.7 Endapo mwanachama atakoma kuwa mwanachama kwa sababu yoyote iliyotajwa hapo juu atarejeshewa asilimia aliyochangia kwenye mali yoyote ya Chama kwa thamani ya wakati huo.

11.8 Mwanachama atakayekoma uanachama kwa kufukuzwa hatapewa nafasi ya kujiunga tena na Chama.

## 12.0 HAKI YA MWANACHAMA

12.1 Kunufaika na Chama kwa mujibu wa Katiba, Kanuni na taratibu za Chama.

12.2 Kukopa kwa mujibu wa taratibu kwa kutegemeana na fedha iliyopo na mahitaji ya wanachama wengine kwa wakati huo.

12.3 Kununua hisa za Chama kwa mujibu wa taratibu na kanuni zilizowekwa.

12.4 Kuuza au kutoa hisa zake wakati wowote ndani ya mwaka wa fedha.

12.5 Bila kuathiri ibara ya 12.4 mwanachama ataruhusiwa kutoa au kuuza jumla ya asilimia thelathini (30) tuu ya hisa zake kwa mwaka. Na endapo ana mkopo hatoruhusiwa kuuza wala kutoa hisa zake kama kiasi cha pesa itakayobaki hiatakidhi masharti ya mkopo wake.

12.6 Haki sawa ya kuchangia mawazo ya uendeshaji wa Chama kwa mujibu wa Katiba, Kanuni na Taratibu.

12.7 Haki ya kupata taarifa za mahesabu na kuhoji matumizi ya pesa za Chama.

## 13.0 MWANACHAMA MPYA

13.1 Bila kuathiri ibara ya 6 na ya 7 ya Katiba hii, Chama kitaendelea kupokea wanachama wapya kulingana na maombi yao ambayo yatapitiwa na wanachama na kuidhinishwa na wanachama Waanzilishi katika mkutano wa mwisho wa wanachama na kama Chama bado hakijafikia idadi ya wanachama ishirini (20).

13.2 Wanachama watatoa mapendekezo ya majina ya waombaji hao ili kujadiliwa kwenye mkutano wa Chama na kudhiriwa na wanachamaWaanzilishi.

13.3 Mwanachama atakayekubaliwa kupokelewa atalipa kiingilio kitakachokubaliwa kwenye mkutano wa wanachama na kuridhiwa na wanachama Waanzilishi. Pamoja na hayo mwanachama atakayekubaliwa kupokelewa atalipa jumla ya michango ya Mfuko wa Jamii yenye thamani ya mwaka mmoja.

13.4 Mwanachama mpya hatapata huduma za Chama kuhusiana na mikopo hadi atakapokuwa ametimiza muda wa miezi sita (6) ndani ya Chama.

13.5 Mwombaji ambaye atakataliwa kwa kutokidhi sifa za uanachama, Chama hakitamfikirkira tena kumpa uanachama katika maisha ya Chama.

## 14.0 UONGOZI WA CHAMA

14.1 Chama kitakuwa na viongozi wafuatao: Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu, Katibu Msaidizi, Mweka Hazina na Mweka Hazina Msaidizi.

14.2 Uongozi wa Chama utachaguliwa kila baada ya miaka mitatu (3) katika Mkutano Mkuu (Annual General Meeting (AGM)).

14.3 Uongozi utachaguliwa kwa kura na/au mapendekezo na kukubaliwa na wote.

## 15.0 MUDA WA UONGOZI

15.1 Uongozi utadumu madarakani kwa muda wa miaka mitatu (3) toka tarehe ya uchaguzi.

15.2 Kiongozi yoyote haruhusiwi kudumu madarakani kwa zaidi ya vipindi viwili mfululizo, yaani miaka sita (6.

15.3 Bali ya kifungu cha 15.2 Kiongozi anaweza kuchaguliwa tena kwa ridhaa (discretion) ya Wanachama.

## 16.0 WAJIBU WA VIONGOZI

16.1 **Mwenyekiti**

a) Ndio Kiongozi na msemaji wa Chama.

b) Ndiye mwendesha Mkutano wa Chama

c) Ndiye msimamizi wa nidhamu ya mkutano na shughuli za Chama.

16.2 **Makamu Mwenyekiti**

a) Ndiye mtekelezaji wa majukumu ya mwenyekiti pindi mwenyekiti anapokuwa hayupo.

b) Ndiye mtekelezaji wa majukumu mengine kama atakavyo pewa na mwenyekiti au mkutano halali wa Chama.

16.3 **Katibu**

a) Ndiye mwandishi wa Mukhtasari wa mkutano.

b) Ndiye mtunza kumbukumbu za mkutano.

c) Ndiye mwandaaji wa agenda na kuitisha mkutano wa Chama.

d) Ndiye mtekelezaji wa majukumu kama atakavyo elekezwa na mwenyekiti au kikao.

e) Ndiye mratibu wa shughuli zote za Chama.

16.4 **Katibu Msaidizi**

a) Ndiye mtekelezaji wa majukumu ya Katibu endapo Katibu hayupo.

b) Ndiye mtekelezaji wa majukumu kama atakavyopangiwa na Katibu na/au mkutano halali wa Chama.

16.5 **Mweka Hazina**

a) Ndiye mtunzaji wa kumbukumbu za fedha za Chama.

b) Ndiye mtoa taarifa ya mapato na matumizi ya Chama.

c) Ndiye msimamizi wa michakato ya mikopo, faini na uwekezaji.

d) Kutengeneza Kanuni za fedha zitakazo pitishwa na wananchama

16.6 **Mweka Hazina Msaidizi**

a) Ndiye mtekelezaji wa majukumu ya Mweka Hazina endapo Mweka Hazina hayupo.

b) Kutekeleza majukumu mengine kama atakavyopewa na Mweka Hazina na mkutano wa halali wa Chama.

## 17.0 UKOMO WA UONGOZI

17.1 Mamlaka ya Kiongozi yoyote wa Chama yatasitishwa ikiwa mojawapo ya mambo yafuatayo yatatokea:

a) Kumaliza kwa muda wa uongozi.

b) Kifo.

c) Kusitishwa uanachama.

d) Kupigiwa kura ya kutokuwa na Imani. Kura hii lazima ziungwe mkono na theluthi mbili (2/3) ya wanachama.

e) Kujiuzulu.

## 18.0 KAMATI TENDAJI

18.1 Kutakuwa na Kamati Tendaji. Kamati Tendaji ni Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina.

18.2 Kamati Tendaji itakutana mara moja kila mwezi.

18.3 Kamati Tendaji itakuwa na majukumu yafuatayo:

a) Kujadili na kuidhinisha maombi ya mikopo.

b) Kutoa taarifa ya maombi ya mikopo kwenye mkutano.

c) Kushughulikia na kutoa mapendekezo endapo kuna masuala yanayowahusu wananchama yanajitokeza.

d) Kujadili mapendekezo na hoja za kusitisha Uanachama kama zitakavyojitokeza.

e) Kupokea, kujadili na kutoa mapendekezo ya Katiba kama itakavyojitokeza.

f) Kujadili na kupendekeza agenda kwa ajili ya mkutano wa mwisho wa mwaka.

g) Na hoja nyingine muhimu.

18.4 Bila kuathiri ibara ya 18.2 ya Katiba hii mkutano wa Kamati Tendaji utatafsiriwa kujumuisha Kamati Tendaji ikikutana ana kwa ana, kufanya mikutano kwa njia

yoyote ile ikiwemo maandishi (circular resolutions), simu na mtandao.

## 19.0 MIKUTANO

19.1 Kutakuwa na mikutano ifuatayo:

a) Mkutano mkuu wa wanachama wote utakaofanyika mara moja kwa mwaka mwezi wa kumi na mbili (Disemba) mwaka wa kalenda. Yani Mkutano wa mwisho wa mwaka wa wanachama wote.

b) Mkutano wa nusu mwaka utakaofanyika kila Julai ya mwaka wa kalenda.

c) Mkutano wa kila mwezi wa wanachama wote.

d) Mkutano wa dharura wa wanachama wote.

19.2 Mkutano mkuu wa wanachama wote utaitishwa na Katibu baada ya kushauriana na Mwenyekiti.

19.3 Mwenyekiti wa Chama atakuwa mwenyekiti wa mkutano mkuu na iwapo hatakuwepo kwa sababu moja ama nyingine, Makamu Mwenyekiti ataongoza mkutano. Iwapo wote hawatakuwepo kwa wakati wote wa kikao, wanachama watamchagua Mweneykit wa Muda kwa ajili ya kuongoza kikao hicho.

19.4 Maamuzi katika mkutano mkuu wa wanachama wote yatafikiwa kwa wingi wa kura za wajumbe waliiohudhuria, endapo kura zitakuwa sawa Mwenyekiti ndiye atakayekuwa na kura ya maamuzi.

19.5 Mkutano wa dharura utaitishwa kwa pendekezo la Mwenyekiti ambalo litaungwa mkono na wanachama wasiopungua nusu ya wanachama hai au pendekezo la wanachama wasiopungua watatu na kuungwa mkono na wanachama wenzao wasiopungua nusu ya wanachama hai.

19.6 Maamuzi katika mkutano wa dharura wa wanachama wote yatafikiwa kwa wingi wa kura za wajumbe waliohuduria.

19.7 Akidi ya mikutano itakuwa idadi isyo pungua nusu ya idadi ya wanachama hai.

## 20.0 FEDHA ZA CHAMA

20.1 Fedha za Chama zitatokana na michango ya wanachama wenyewe, riba ya benki, riba ya mikopo ya wanachama, faini za aina zote, misaada kutoka taasisi mablimbali na kutokana na miradi ya uzalishaji mali itakayoendeshwa na Chama.

## 21.0 AINA ZA MICHANGO

21.1 Kila mwanachama atalazimika kuchangia kama ifuatavyo:-

a) Kiingiio

b) Mfuko wa Jamii wa kujiunga

c) Hisa

21.2 Kila mwanachama ana haki ya kununua hisa kila mwezi.

21.3 Bila kuathiri ibara hii ni lazima kila mwanachama kununua hisa walau ya thamani ya Shilingi laki moja (Tshs.100,000/-) kama kiwango cha chini kila mwezi.

21.4 Malipo ya hisa ya kila mwezi, fedha za mfuko wa Jamii, faini na malipo mengineyo yoyote yatalipwa kabla au siku ya tarehe 5 ya kila mwezi. Baada ya tarehe 5 kutakuwa na faini.

21.5 Kiwango cha faini, cha Jamii, cha uwekezaji, nk, itajadiliwa katika Mkutano mkuu wa kila mwaka.

21.6 Michango yote ya Chama itawekwa katika akaunti za Chama na mwanachama husika atalazimika kuleta uthibitisho wa malipo hayo kwa Mweka Hazina kwa ajili ya uthibitisho na kumbukumbu.

21.7 Mwanachama atawajibika kuweka fedha katika akaunti husika za Chama na kumpatia uthibitisho Mweka Hazina na sio pesa taslimu.

21.8 Fedha za Chama zitatunzwa kwenye akaunti zitakazofunguliwa katika benki au mfumo wa elektroniki (mfano M-KOBA nk.), utakaoamuliwa na wanachama.

21.9 Fedha zote za mfuko wa Jamii hazitatumika katika kukopeshana au kufanyia shughuli zisizo za mfuko wa Jamii.

## 22.0 MIKOPO

22.1 Pamoja na utaratibu utakaowekwa na Kamati Tendaji, fedha za Chama zitakopeshwa kwa wanachama kwa mujibu wa kanuni na taratibu zilizopo.

22.2 Kila mwanachama atakayetaka kukopa lazima awe na wadhamini wawili ambao nao lazima wawe wanachama hai.

22.3 Endapo mkopaji atakuwa sio mwanachama atapaswa kuwa na mdamini ndani ya Chama pamoja na dhamana. Hisa ndiyo dhamana.

22.4 Mizania ya chini ya akaunti ya Chama kwa pesa ambazo sio za mfuko wa Jamii itakuwa si chini ya Shilingi million mbili (Tshs.2,000,000/-).

22.5 Tozo ya riba ya mkopo itakuwa kwa mujibu wa kanuni zilizoainishwa na Chama kwa mujibu wa Katiba hii.

22.6 Iwapo mwanachama atashindwa kuwasilisha marejesho ya mkopo pamoja na riba kwa miezi mitatu mfululizo bila ya sabau za msingi na baada ya jitihada za kurejesha fedha zote zinazodaiwa ndani ya muda aliopewa kushindikana, Kamati Tendaji itamuamuru kurejesha pesa zote anazodaiwa pamoja na riba ndani ya mwezi mmoja na Chama kitafanya maamuzi ya uanachama wake.

22.7 Endapo mwanachama atashindwa kutekeleza sharti lililopo katika ibara ya 22.6 ya Katiba hii atafukuzwa Uanachama na wadhamini wake kutakiwa kulipa deni (mkopo na riba) ndani ya miezi mitatu toka siku ya maamuzi ya uongozi wa Chama. Ikishindikana

itabidi wadhamini warejeshe kiasi husika kutokana na hisa zao au vyanzo vingine. Kwa mkopo wa nje mwanachama mdhamini atalipa ila hataondolewa uanachama.

## 23.0 MIRADI AU SHUGHULI ZA CHAMA

23.1 Miradi ya Chama itaendeshwa kutokana na maamuzi ya mkutano halali wa Chama.

23.2 Chama kwa makubaliano wa wanachama waanzilishi kinaweza kufungua shuguli nyingine za kiuchumi au za kijamii (kuisaidia jamii, yaani shughuli za isani (charity work)).

## 24.0 MALI ZA CHAMA

24.1 Chama kitanunua mali kwa jina la Chama au itakavyoamuliwa na waanzilishi wa Chama.

24.2 Chama kinaweza kupata mali kwa njia ya:

a) Kupewa zawadi

b) Kununua

c) Kukopa

d) Kurithishwa

## 25.0 KUVUNJWA KWA CHAMA

25.1 Chama kitavunjwa kwa:

a) Makubaliano ya theluthi mbili (2/3) ya wanachama.

b) Kwa mujibu wa Sheria za nchi.

25.2 Chama kitatengeneza kanuni itakayotumika endapo Chama kitavunjwa.

## 26.0 MABADILIKO YA KATIBA

26.1 Katiba hii ni ya kudumu lakini itakuwa inafanyiwa marekebisho mara kwa mara kulingana na wanchama watakavyoona inafaa katika mkutano mkuu.

26.2 Mabadiliko yoyote ya Katiba hii yatafanywa na mkutano mkuu wa wanachama na yanapaswa kuungwa mkono na theluthi mbili (2/3) ya wanachama waliohudhuria.

26.3 Akidi ya mkutano mkuu au mkutano wa dharura wa wanachama kwa minajili ya kubadili Katiba itakuwa si chini ya robo tatu (3/4) ya wanachama.

26.4 Kwa mujibu wa Sheria za nchi.

## 27.0 LUGHA YA KATIBA

27.1 Lugha rasmi ya Katiba hii itakuwa Kiswahili, lakini inaweza kutafsiriwa kwa lugha nyingine yoyote pale itakapohitajika.

## 28.0 MIGOGORO

28.1 Migogoro yote itakayojitokeza ndani ya Chama itatatuliwa kwa njia ya usuluhishi kwa njia ifuatayo:

a) Kwamba punde mgogoro utakapo tokea utawasilishwa kwa Kamati Tendaji ndani ya siku kumi

na nne (14) kwa maridhiano (mediation au amicable settlement) na Kamati Tendaji kuutatua mgogoro husika ndani ya siku arobaini (40).

b) Pale ambapo mgogoro umeshindikana kupata maridhiano basi utasuluhishwa kwa njia ya Usuluhishi (Arbitration) kwa kutumia chombo cha Tanzania Institute of Arbitrators (TIArb), kwa kutumia Kanuni za TIArb na kwa njia ya Msuluhishi (Arbitrator) mmoja na kufanyika hapa Dar es Salaam kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

**Katiba hii imepitishwa na Wanachama waanzilishi kwa kuweka majina yao na sahihi zao kwenye Katiba hii leo Tarehe <u>12 Januari 2024</u> kama ifuatavyo:**

| No. | JINA KAMILI | WADHIFA | SAHIHI |
|---|---|---|---|
| 1. | BIBIE UWESU MSSUMI | MWENYEKITI NA<br><br>MWANACHAMA | |
| 2. | SARAH RASHID KINYAGA | MAKAMU MWENYEKITI NA<br><br>MWANACHAMA MUANZILISHI | |
| 3. | HAPPINESS WERIMEKI MCHAKI | KATIBU NA<br><br>MWANACHAMA MUANZILISHI | |
| 4. | DORA ALBERT KYUNGU | MWEKA HAZINA NA<br><br>MWANACHAMA | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | MUANZILISHI | |
| 5. | BAHATI NDESERUA MOSHI | MWEKA HAZINA MSAIDIZI NA<br><br>MWANACHAMA MUANZILISHI | |
| 6. | NEEMA NICHOLAUS CHUSI | MWANACHAMA MUANZILISHI | |
| 7. | SEKELA POLISYA MWAISEJE | MWANACHAMA MUANZILISHI | |
| 8. | DYNESS REDSON LYIMO | MWANACHAMA MUANZILISHI | |